



Hakika ilikuwa inakutosheleza kupiga kwa mikono yako hivi" Kisha akapiga kwa mikono yake miwili chini ya ardhi mpigo mmoja, kisha ukapaka mkono wa kushoto juu ya mkono wa kulia, na juu ya viganja vyake na uso wake

Kutoka kwa Ammari Bin Yasiri radhi za Allah ziwe juu yake amesema: Aliniagiza Mtume - Rehema na Amani ziwe juu yake- katika haja fulani, nikapatwa na janaba, nikawa sikupata maji, nikajigaragaza katika udongo kama anavyojigaragaza mnyama, kisha nikamuendea Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- Nikamsimulia hilo, akasema: "Hakika ilikuwa inakutosheleza kupiga kwa mikono yako hivi" Kisha akapiga kwa mikono yake miwili chini ya ardhi mpigo mmoja, kisha ukapaka mkono wa kushoto juu ya mkono wa kulia, na juu ya viganja vyake na uso wake".

[Sahih] [Wamekubaliana Bukhaari na Muslim]

Alimtuma Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- Ammari Bin Yasiri radhi za Allah ziwe juu yake katika moja ya safari kwa baadhi ya haja zake, akapatwa na janaba kwa tendo la ndoa au kushukwa na manii kwa matamanio, na hakupata maji ili aoge, Na alikuwa hajui hukumu ya tayamam kwa ajili ya janaba, bali alikuwa anajua hukumu yake kwa hadathi ndogo, akajitahidi na akadhani kuwa kama ambavyo hufuta kwa udongo baadhi ya viungo vya uduh kwa kuondoa hadathi ndogo, akaona kuwa kutayamam kwa kuondoa janaba ni lazima aeneze udongo mwili mzima; kwa kuchukulia kipimo katika maji, akajigeuzageuza katika udogo mpaka akaueneza mwili mzima na akaswali, alipokuja kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-, akamueleza kuhusu hilo; ili aone je yeye amepatia au amekosea? Akambainishia Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- namna ya kujitwaharisha kutokana na hadathi mbili, ndogo kama haja ndogo, na hadathi kubwa kama janaba: Nako ni mtu kupiga kwa mikono yake miwili juu ya udongo mpigo mmoja, kisha afute kwa mkono wa kushoto juu ya mkono wa kulia, na juu ya viganja vyake na uso wake.

النّجّات الخيريّة
ALNAJAT CHARITY

